**TEOFILO KISANJI UNIVERSITY**

**TEKU Journal of Interdisciplinary Studies (TJIS)**

**ISSN 3057-3351 (Print) & ISSN 2738-9006 (Online)**

**Journal Homepage: https://www.teku.ac.tz/tjis.php**

**Makala ya Kiutafiti**

# Uchanganuzi wa Ruwaza za Toni katika Vitenzi Visoukomo Sahili vya Kirombo

Peter T Mramba

*Chuo Kikuu cha Mt. Augustino, Ndaki Shiriki Jordan Morogoro, Tanzania*

*Correspondence: mrambadoctor@gmail.com*

**MAELEZO YA MAKALA**

*Kupokelewa:* 23-Agosti-24

*Kurekebishwa:* 20-Novemba-25

*Kukubaliwa:* 20-Februari-25

*Kuchapishwa mtandaoni:* 30-Machi-25

*DOI:* 10.70055/TJISV4I2A06

*Copyright:* The Author(s) (2025)

*Publisher:* Teofilo Kisanji University

*Licence:* This is an open access article under the CC BY 4.0

**IKISIRI**

Makala haya yanahusu uchanganuzi wa ruwaza za Toni katika Vitenzi visoukomo sahili vya Kirombo. Lengo kuu la makala haya ni kuchunguza ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika vitenzi visoukomo sahili vya Kirombo na kanuni zinazotawala utokeaji huo. Aidha, malengo mahususi: kubainisha silabi inayohusishwa na Tonijuu Msingi (kuanzia sasa TJM) na mbili, kujadili ruwaza ya utokeaji wa toni katika vitenzi visoukomo sahili vya Kirombo na kanuni zinazotawala hutokeaji huo. Data ya Makala haya imetokana na utafiti mpana uliofanywa juu ya toni katika lugha ya Kirombo wilayani Rombo (2023) ambao uliongozwa na Nadharia ya Fonolojia Vipandesauti Huru kwa kutumia Mkabala wa Tonijuu Msingi kama ulivyoasisiwa na Goldsmith (1976) na kuboreshwa na wanazuoni mbalimbali katika taaluma ya tonolojia. Aidha, mbinu za ukusanyaji data zilizotumika ni pamoja na mahojiano na ushuhudiaji. Katika mahojiano vitenzi visoukomo sahili viliandaliwa kwa Kiswahili na watoataarifa walihitajika kuvitamka kwa Kirombo huku mtafiti akirekodi na kualamisha toni katika vitenzi hivyo. Aidha, katika mbinu ya ushuhudiaji Mtafiti alishuhudia kwa kushiriki. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, kuna ruwaza mbalimbali za kitoni zinazoleteleza utokeaji wa kanuni za kitoni ambazo hutofautiana kutegemeana na idadi ya silabi. Ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika vitenzi visoukomo sahili vya silabi mbili hadi sita, TJM hupachikwa katika silabi ya pili ya shina kutoka mwanzoni mwa neno. Aidha, kanuni anuwai kama vile usambaaji wa TJM kuelekea kulia mwa shina la kitenzi, uhamaji wa TJM, uradidi wa TJM na Udondoshaji wa kitamkwa, zimetekelezwa baada ya utekelezwaji wa kanuni ya jumla ya Upachikaji wa TJM, katika uibuzi wa ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani. Aidha, ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika vitenzi vya idadi ya silabi mbili hadi sita vyote huanza na toni C katika KA ikifuatiwa ama na toni J au toni C katika silabi ya kwanza ya shina. Toni J hiyo usambaa hadi silabi ya mwisho kasoro mbili au moja kutoka mwishoni mwa shina la vitenzi husika.

## 1. Utangulizi

Lugha za binadamu ulimwenguni zina sifa ya kuwa na vipambasauti (Massamba, 2011). Hivi ni vipengele vya uchanganuzi arudhi viwezavyo kuandamishwa kwenye vitamkwa. Vipengele hivi ni pamoja na toni, mkazo, usilabi, kidatu, unazali, unguvunguvu, na nguvumsikiko. Makala haya yanahusika na kipengee cha toni ambacho ni kipambasauti chenye uamilifu wa kileksika na kisarufi kinachoweza kupambanua maana za maneno na kuwakilisha njeo (Odden, 2005; Massamba, 2011: 171; Batibo, 2012). Kwa mujibu wa wataalamu Heine na Nurse (2000), Nurse na Philipson (2003) na Batibo (2012), lugha nyingi za Kiafrika zina toni, ukiondoa zile za kundi la lugha za Kihamitiki kama vile Kishemu/Kihamu. Toni ni miongoni mwa sifa za kiarudhi[1] zilizowahamasisha wanaisimu kuchunguza vipengele mbalimbali vya lugha za Kibantu kwa kutumia Nadharia za taaluma ya fonolojia (Hyman, 2008). Suala la uwakilishi wa toni katika lugha lilishamiri zaidi hasa pale mwanaisimu Goldsmith (1976) alipoonesha mwanga wa uchanganuzi wa toni katika lugha mahususi kwa kutumia Nadharia

[1] *Arudhi ni sifa inayohusu mabadiliko ya vipambasauti kama vile kidatu, nguvumsikiko, tempo na lahani (Massamba, 2012).*

ya Fonolojia Vipandesauti Huru kama maboresho ya Nadharia ya Fonolojia Zalishi (Hayman, 2003: 4-6 na Massamba, 2011: 178).

## 2. Lugha ya Kirombo

Kirombo ni lugha ya Kibantu iliyopo miongoni mwa jamiilugha za Kichaga. Kichaga hakina lugha moja inayoweza kuunganisha jamii ya Wachaga wote. Kila eneo (tarafa) lina lugha yake na kila kata ndani ya tarafa ina matamshi yake (Mramba, 2015). Kwa mujibu wa MLUTA (2009), jamii ya Wachaga ina jumla ya lugha asilia sita zinazotumika kwa mawasiliano ndani na nje ya eneo kitovu (Kilimanjaro). Lugha hizo ni *Kirombo, Kimachame, Kikahe, Kihusa, Kimochi na Kisia.* Hata hivyo, kuna lahaja zinazozungumzwa ndani ya jamii ya Wachaga kama vile Kiuru, Kiwoso, Kivunjo, Kichasu, Kimarangu na Kihanjo.

Kutokana na tafiti zilizofanywa na wataalamu mbalimbali kama Raum (1964), Polomé (1971), Van Spaandock (1971), Nurse na Philipson (1977), Heine na Nurse (2003), Martinet (2005), McHugh (2006), na Nelson (2013) katika lugha za Kichaga kama vile Kiold Mochi, Kimachame, Kivunjo, Kikahe na Kisiha, wamebaini kuwa lugha hizo zina toni. Aidha, wamebaini mabadiliko ya utokeaji wa ruwaza za toni katika lugha hizo hayapo sawa jambo linalofanya baadhi ya lugha kuwa na zaidi ya 66% ya tonichini na chini ya 34% ya tonijuu katika maneno yake. Kulingana na matokeo ya tafiti hizo na ikizingatiwa kwamba Kirombo ni miongoni mwa jamii lugha za Kichaga, Kirombo pia kina toni ingawa haikuelezwa ruwaza yake ya utokeaji ikoje hususani kwa vitenzi visoukomo sahili.

Aidha, Kirombo kinadhihirisha wazi kina toni kulingana na ruwaza za maneno yake ambayo kiothografia huonekana sawa ilhali wazawa wa lugha hiyo wanapoyatumia katika mazungumzo yao huchomoza maana tofauti. Tutazame mfano (1) hapa chini:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | a) | ílya | ‘kula’ |
| | | ilyá | ‘kukataa’ |
| | b) | íla | ‘kulala’ |
| | | ilá | ‘kuita’ |

Hivyo, katika 1(a) tunaona mambo yafuatayo: tonijuu ikijitokeza katika silabi ya kwanza ya neno maana yake huwa ‘*kula*’ na maana hubadilika na kuwa ‘*kukataa*’ toni inapojitokeza katika silabi ya pili ya neno. Hali hiyo inajitokeza katika 1(ii) kama inavyoonekana hapo juu. Pia, toni katika Kirombo hubadili kategoria ya maneno kama inavyoonekana katika mfano wa 2:

| | | |
|---|---|---|
| 2. | a) i-kerésa | gereza (N) |
| | i-kéresa | chonga kitu (T) |
| | b) sháa | nje (N) |
| | shaá | beza /kataa (T) |
| | c). i-sháa | kuja (T) |
| | i-shaá | ukucha mkubwa (N) |
| | d). i- káa | kaa la moto |
| | i-kàa | kukaa/kuishi mahala fulani (T) |

Katika 2 (a) tunaona mambo yafuatayo: tonijuu ikijitokeza katika silabi ya pili ya shina la neno huwa na maana ya gereza (N), wakati ikihamia silabi ya kwanza ya shina huwa na maana ya chonga kitu (T). Halikadhalika, katika (b) tonijuu ikiwa katika irabu ya kwanza ya shina huwa na maana ya nje (N) na ikihamia kwenye silabi ya pili huwa na maana ya beza/ kataa (T). Hali hiyo inajitokeza pia katika mfano wa (c), ila katika mfano wa (d) tonichini ikitokea mahala pa tonijuu pia maana na kategoria hubadilika kama inavyoonekana.

Hii inatokana na ukweli kwamba lugha nyingi za Kibantu zina toni hususani zile za kundi la Naija-Kongo ambapo Kirombo hupatikana humo (taz. Nurse na Philipson, 2003). Batibo (2012) akimnukuu Van Spaandock (1971), anasema, kiasili jamiilugha za Kichaga zina toni, ambapo katika kila silabi na kila neno huwa na toni maalumu. Kutokana na maelezo hayo tunajiuliza: je, TJM katika vitenzi visoukomo sahili huhusishwa na silabi ipi? Je, ruwaza ya toni katika vitenzi visoukomo sahili katika Kirombo ikoje na hutawaliwa na kanuni zipi? Maswali haya na mengine mengi tuliyokuwa tukijiuliza, yamejibiwa vyema katika sehemu ya 5.0 ambapo ruwaza za ujitokezaji wa toni kuanzia silabi chache hadi nyingi kiidadi za mashina ya vitenzi visoukomo sahili zimechanganuliwa.

## 3. Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Fonolojia Vipandesauti Huru. Nadharia hii imeasisiwa na Goldsmith (1976). Wazo kuu la nadharia ya Fonolojia Vipandesauti Huru (Kuanzia sasa FVH) ni kuwa, vipengee vyote vya kifonolojia, kikiwemo kipambasauti toni havina budi kuchukuliwa kuwa viko huru katika usemaji wa lugha yoyote iwayo. Vipengee hivyo vinapaswa kuchukuliwa katika upekee wake wa kujitegemea na kuwakilishwa kama vitu vilivyo huru lakini vinavyohusiana.

Katika kufanikisha hilo vipengee vyote huwakilishwa kwa kutumia rusu, yaani rusu ya vipandesauti, rusu ya kiimbotoni, rusu ya toni, na kadhalika. Rusu hizo huhusishwa kwa mistari ya uhusiano ambayo hudhibitiwa na Sharti la Ukubalifu linalodai kwamba, kila irabu ihusishwe na angalau toni moja, kila toni ihusishwe na angalau irabu moja, na mistari ya uhusiano isikingamane. Ukiukwaji wa sharti la ukubalifu huleteleza maumbo yasiyokubalika katika lugha husika. Nadharia ya FVH ina mikabala miwili ya uchanganuzi wa kipambasauti toni ambayo ni; mkabala wa uchanganuzi wa kiinitoni ambao huchombeza toni juu na mkabala wa Tonijuu Msingi kama msingi wa uchanganuzi wa toni. Katika Makala haya mkabala wa Tonijuu Msingi ndio uliotumika.

Mkabala wa Tonijuu Msingi (JM) hutumia toni juu (J) kama msingi wa uchanganuzi wa toni. Toni J huwekwa ama chini au juu ya irabu inamojitokeza. Mkabala huu ni matokeo ya kuboreshwa kwa mkabala wa Kiinitoni kama msingi wa uchanganuzi wa toni uliasisiwa na Goldsmith (1976), na kutumiwa na wataalamu wa isimu kama Massamba (1984), Ismail (2011, na 2016), na Mashauri (2012). Mkabala wa JM unazingatia uchanganuzi wa toni kwa kutumia Tonijuu Msingi (JM) katika kupata umbo la nje linalokubalika na wasemaji wazawa wa lugha. Vipengee vyote huwakilishwa kwa kutumia rusu zinazohusishwa kwa mistari ya uhusiano ambayo hudhibitiwa na Sharti la Ukubalifu kama ilivyo kwa mkabala wa uchanganuzi wa kiiinitoni kinachochombeza toni (KT). Miongoni mwa wanaisimu wanaotumia mkabala wa JM ni pamoja na Marlo (2007), Batibo (1990), Odden (1989), Ismail (2016), Hyman na Byarushengo (1984) kwa kutaja tu wachache. Mkabala wa JM umeteuliuwa kukokotoa ruwaza ya utokeaji wa toni katika vitenzi visoukomo sahili kwa sababu uchanganuzi wake huleta uwazi zaidi katika ujitokezaji wa umbo la nje, upunguza idadi ya rusu katika ukokotozi wa umbo la nje kutoka umbo la ndani, ukilinganisha na mkabala wa Kiinitoni katika uchanganuzi wa toni kwa kutumia kiinitoni kinachochombeza toni juu.

## 4. Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti ni njia ambazo hutumiwa na mtafiti katika kukusanya na kuchakata data. Mbinu hizi humwezesha mtafiti kupata data sahihi za utafiti, kuchagua mkabala, sampuli na vifaa ambavyo atatumia katika utafiti wake (Kothari, 2010). Aidha, Nshubemuki (2004), mbinu za utafiti ni hatua au njia za makusudi zifanywazo na mtafiti ili kukwepa kujidanganya au kuwadanganya wengine watakaosoma ripoti yake. Aidha, mbinu zilizotumika ni pamoja na mahojiano na ushuhudiaji. Katika mahojiano vitenzi visoukomo sahili viliandaliwa kwa Kiswahili na watoataarifa walihitajika kuvitamka kwa Kirombo huku mtafiti akirekodi na kualamisha toni katika vitenzi hivyo. Watoataarifa waliombwa ridhaa ya kurekodiwa kwa kuelezwa umuhimu wake katika utafiti huu kabla ya kufanya hivyo. Aidha, katika mbinu ya ushuhudiaji Mtafiti alitembelea vijiwe viwili vya karata, ambapo wazee hupatikana majira ya jioni baada ya shughuli zao za kutwa. Mtafiti alishuhudia kwa kushiriki. Yaani, alishiriki kucheza karata kama sehemu ya timu au kundi pinzani. Kwa kufanya hivyo, ilikuwa rahisi kupata data sahihi ya matamshi kwa sababu watoa taarifa walikuwa huru kuzungumza wao kwa wao bila kujiandaa kutamka kitenzi fulani.

Data iliyokusudiwa katika utafiti huu ni vitenzi visoukomo sahili 150 vya Kirombo vinavyodhihirisha ruwaza za ujitokezaji wa toni ambayo ilipatikana baada ya mtafiti kuchambua taarifa zilizotolewa na watoataarifa kwa njia ya mahojiano na ushuhudiaji kutoka uwandani. Mbinu mwafaka za uteuzi wa maneno zilizingatiwa kama msingi wa kupata matokeo jumuifu, sahihi na kubalifu. Moja ya mbinu hizo ni kugawa maneno katika makundi kwa kuzingatia idadi ya silabi za shina la kitenzi na ruwaza za ujitokezaji wa toni katika vitenzi husika. Mbinu za utafiti zilihusisha mahojiano na ushuhudiaji kulingana na aina ya utafiti uliofanyika. Mfano wa vitenzi visoukomo sahili vya Kirombo vilivyotajwa na watoataarifa kupitia mbinu ya usaili ni kama inavyoonekana katika (3) ambapo mtafiti aliandaa orodha ya vitenzi visoukomo sahili vya Kirombo kisha kuwataka watoataarifa kutamka mmojammoja ili kupata ruwaza sahihi ya ujitokezaji wa toni katika vitenzi husika. Mfano wa vitenzi walivyopewa vinaonekana katika 3a na 3b:

3a. Mfano wa vitenzi: *a) iseka* *'kucheka'*
*b) iterefa* *'kuomba'*
*c) iboryomwa* *'kubomoka'*
*d) idishirya* *'kukimbizia'*

Baada ya kutamka matokeo yake yalionekana kama ifuatavyo katika 3a hapa chini:

3b. a*) iséka* *'kucheka'*
*b) itéréfa* *'kuomba'*
*c) ibóryómwa* *'kubomoka'*
*d) idíshírya* *'kukimbizia'*
Chanzo: (Uwandani, 2023).

Matokeo ya 3b hapo juu yanaonesha namna ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika vitenzi vya Kirombo ilivyopatikana kwa kutumia njia ya mahojiano. Aidha, kupitia mbinu ya ushuhudiaji mtafiti alibaini ruwaza ya utokeaji wa toni katika vitenzi visoukomo sahili vya Kirombo kama inavyoonekana katika (4);

4. *……. isána isóryo na iféle……. '…kuokota jike na dume…'*
*…idúmbwa ibúrya aróbo stíni… '…kukata kucheza robo sitini…'*
*…isínyána na ikúrána ibúrya…'….kukonyezana na kugusana kucheza…'*
*…..isóryómólyána isóryo na matífi ya mbúru…'kuchomoleana dume na kitanda…..'*
*……imúlémbérya írya idúryúfu na ktárya ílyi imwályíkya iféle… '…..kumchomekea kuchukua jembe na kitanda ili kumwolea jike……*

Chanzo: (Uwandani, 2023).

Data ya (4) hapo juu ilipatikana kupitia mazungumzo ya kawaida ya wazee ambao ni wazungumzaji wazawa wa Kirombo. Data ya (4) inaonesha namna ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika vitenzi visoukomo sahili vilivyopatika kupitia njia ya ushuhudiaji ambayo mtafiti alikusudia kupata data sahihi bila mtoataarifa kutamka neno moja moja au kujipanga kuzungumza.

## 5. Ruwaza za Toni katika Vitenzi Visoukomo Sahili vya Kirombo

Katika sehemu hii tumechunguza jinsi ruwaza ya toni inavyojitokeza katika vitenzi visoukomo sahili vya Kirombo. Ili kufanikisha hilo, tumechunguza vitenzi visoukomo sahili kwa kuzingatia idadi ya silabi katika kitenzi husika. Yaani, kwa kuanza na vile vyenye muundo wa silabi chache hadi vile vyenye idadi ya silabi nyingi.

Pamoja na hayo, tulieleza tutatumia mkabala wa Tonijuu Msingi katika uibuzi wa ruwaza ya toni kutoka umbo la ndani kwenda umbo la nje la vitenzi visoukomo sahili vya Kirombo. Katika kufanya hivyo tunapaswa kujua, tonijuu msingi (kuanzia sasa TJM) inahusishwa na silabi ipi katika kitenzi kisoukomo sahili? Ama kwa hakika hapa hakuna jibu la mkato. Hii hutokana na ukweli kwamba, kila lugha ina taratibu zake maalumu za upachikaji wa TJM katika mashina ya vitenzi au maneno mengine.

Kabla ya kuendelea na mjadala wa kutaka kujua TJM huhusishwa na silabi ipi katika lugha ya Kirombo, yafaa tufafanue hapa lau kwa kina kwanza tunaposema TJM tuna maanisha nini ndipo tuendelee na mjadala wetu. Lugha nyingi za Kibantu katika miaka ya 500 baada ya Kristu zilionekana kuwa na toni mbili tofauti ambazo ni tonijuu (J) na tonichini (C) (Meeussen, 1980; Coupez, 1983; Marlon a Odden, 2014 na Hyman, 2017). Utofauti wa toni hizo umetokana na kuwa na viwango tofauti kimsikiko. Yaani, Tonijuu (kuanzia sasa J) ni toni ambayo silabi inayohusishwa nayo inapotamkwa huwa ina msikiko unaoelekea juu, wakati tonichini (kuanzia sasa C) ni toni ambayo silabi inayohusishwa nayo inapotamkwa msikiko unaelekea chini (Massamba 2011: 171, Möller, 2014:12). Toni J hualamishwa kwa alama [ ´ ] na toni C hutumia alama [ ` ].

Hata hivyo, wapo wataalamu wanaoona kuwa awali lugha za Kibantu zilikuwa na toni J moja na toni kapa (ø) (toni J Vs ø) (Stevick, 1969 na Nash, 1992). Wataalamu hawa hudai kuwa toni kapa kimsikiko ni hafifu sana na hivyo kuona kuwa haipo. Madai ya kundi hili kwa hakika hayasigani na madai ya kundi la kwanza kwa sababu wote wanatambua kuwa awali lugha za Kibantu zilikuwa na viwango viwili tofauti vya toni na ambavyo vilitofautishwa kulingana na msikiko kiutamkaji.

Kwa kuwa imekwisha elezwa kwamba toni J na toni C ndizo toni pekee zilizokuwepo awali katika lugha nyingi za Kibantu kabla ya utokeaji wa mabadiliko ya Kiisimu katika lugha hizo, na ambazo zikiungana matokeo yake ni uzalishaji wa ama toni TP au toni TS, basi toni J na toni C, zote uchukuliwa kuwa ni Toni Msingi katika lugha za Kibantu. Kwa kuwa toni J msingi imebainika kuwa na mvumo wa juu kimsikiko kuliko toni C, na kwa kuwa baadhi ya

 TJIS, Vol.4, Issue 2 (December 2024) pp. 50-62 DOI: 10.70055/TJISV4I2A06

wataalamu wanaiona toni C kama toni kapa (ø) na ambayo mara nyingi haialamishwi inapotokea na toni J katika neno moja, basi tunachukulia kifonolojia toni J ndiyo msingi wa toni zote katika lugha.

Kutokana na maelezo ya kinadharia yaliyotolewa hapo juu, uchanganuzi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani katika Kirombo utatumia toni J kama toni msingi (TJM). Kwa mujibu wa Moller (2014), Toni Msingi huweza kujidhihirisha kwa namna tofauti kwenye maneno mbalimbali. Kwa kawaida maneno hubeba sauti na toni msingi inayohusishwa na silabi maalumu. Pia, neno linaweza kusitiri toni msingi bila kuhihusisha na silabi. Ikitokea hivyo, neno husika litakuwa na toni inayoelea. Aidha, lugha inaweza kuwa na maneno yasiyo na toni msingi na hivyo kufanya maneno hayo kuitwa *maneno yasiyo na toni*. Ni mara chache sana kukuta lugha yenye kusitiri aina zote za maneno yenye aina hizo za toni msingi zilizotajwa (Snider, 1999:6). Tuchunguze kiolezo kifuatacho katika 2a;

2a) **Neno lenye toni na silabi** b) **Neno lenye toni inayoelea** c) **Neno lisilo na toni**

```
        T                       T
        |
       #$#                     #$#                 #$#
```

Alama (T) imetumika kama toni, alama ($) imetumika kama silabi na alama (#) imetumika kuonesha mwanzo na mwisho wa neno. Ukichunguza violezo vilivyopo katika 90 hapo juu utabaini kwamba, kiolezo cha 2(a)kina toni msingi iliyohusishwa na silabi maalumu kwenye neno, wakati kiolezo cha 2(b) kinaonesha kuwa kina toni msingi inayoelea kwa sababu haijahusishwa na silabi maalumu katika neno na mwisho kiolezo cha 2(c) kinaonesha neno ambalo halina toni msingi na hivyo kuwa neno lisilo na toni.

Katika lugha ya Kirombo toni msingi hujitokeza kwa namna ya kwanza iliyotajwa na Moller (keshatajwa) ambapo TJM huhusishwa na silabi maalumu kwenye kitenzi katika umbo la ndani, kwa kufuata utaratibu unaofanana kwa vitenzi visoukomo sahili vyote vya lugha inayohusika. Ili tuweze kujua ni silabi ipi katika kitenzi huhusishwa na TJM katika Kirombo, hatuna budi kufanya uchanganuzi wa kimajaribio utakaoongozwa kwa kanuni maalumu. Tunapendekeza kanuni itakayotumika katika upachiaji wa toni J msingi kwenye silabi maalumu ya shina la kitenzi kisoukomo kuwa ni *kanuni ya jumla ya upachikaji wa toni J msingi katika silabi maalumu ya shina la kitenzi kisoukomo*. Kanuni hii imeundwe baada ya kufanyika kwa majaribio anuai ambayo ndiyo yaliyotupatia idhibati kuwa TJM hupachikwa kwenye silabi ipi.

Katika kufanya hivyo, tumechukua kitenzi kisoukomo sahili cha silabi mbili za shina katika lugha ya Kirombo '**itéma** '*kulima*' na kukifanyia majaribio mbalimbali ya kiukokotozi hadi kubaini TJM hupachikwa katika silabi ya kwanza ya shina la kitenzi. Ambapo, mtafiti alianza kupachika JM katika silabi ya mwisho ya shina la kitenzi kisoukomo husika ambapo alipata matokeo yasiyokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wazawa wa Kirombo [* i te má]. Mtafiti aliaisha JM kutoka silabi ya mwisho wa shina kisha kuipachika katika silabi ya kwanza ya shina la kitenzi '**itéma**' ambapo ukokotozi huo ulitoa matokeo yanayokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wazawa wa Kirombo [i té ma] kama inavyoonekana hapa chini.

Ukokotozi wa jaribio la (2) hapo juu, umetupatia matokeo yanayokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kirombo. Matokeo ya ukokotozi huu yanaonesha kuwa, TJM hupachikwa katika silabi ya kwanza ya shina la kitenzi kisoukomo [*i té ma*]. Ukichunguza kwa umakini matokeo haya ya ukokotozi utagundua kwamba kiambishi awali (kisoukomo) cha kitenzi hicho kimebeba toni C, ikifuatiwa na toni J ya silabi ya kwanza ya shina na kisha kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina. Katika ukokotozi huu hatuhitaji kutekeleza kanuni yoyote ya Sharti la Ukubalifu kwa sababu limefanyika tayari katika hatua ya uhusishaji wa tonichini na vitamkwa. Kwa kutumia matokeo ya ukokotozi wa jaribio hili la (2), tunaweza kuhitimisha kwamba, TJM hupachikwa katika silabi ya kwanza ya shina la kitenzi kisoukomo katika lugha ya Kirombo. Hata hivyo, kama haitoshi tumejiridhisha zaidi kwa kufanya jaribio linginge kwa kutumia kitenzi kisoukomo sahili cha silabi tatu za shina **itéréfa** '*kuomba*'ambacho kina toni C katika kiambishi awali (kisoukomo) / i-/, toni J mbili zinazofuatana kuanzia silabi ya kwanza hadi silabi ya pili ya shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina. Tumeteua kitenzi hiki kwa sababu kina toni J mbili zinazofuatana katika silabi mbili za shina moja. Pamoja na mfuatano huo tulitaka kujiridhisha kama inawezekana TJM ikapachikwa katika silabi ya pili ya shina kwa kuwa nayo imebeba toni J kama ilivyo kwa silabi ya kwanza ya shina. Matokeo ya ukokotozi wa kitenzi **itéréfa** '*kuomba*' bado yameonesha kuwa TJM hupachikwa katika silabi ya kwanza ya shin a hata kama neno litakuwa na toni J zaidi ya moja kwenye silabi za shina la kitenzi zinazofuatana.


```
        itéma              'kulima'
        /i te ma /         'Umbo la ndani'
           J
           |
2.       i te ma           Upachikaji TJM
          C  J  C
          |  |  |
          i te ma          'Uhusishaji wa tonichini na Vitamkwa'
         [i té ma]         'Umbo la nje'
```

Pamoja na hayo majaribio tuliyofanya hapo juu, matokeo yake ya uhusishaji wa TJM yametuwezesha kuunda kanuni ya upachikaji wa TJM kwenye vitenzi visoukomo sahili vya Kirombo kama ifuatavyo: (ambapo; KA = Kiambishi Awali (kisoukomo) na SH = shina. Pia, alama ya dola [$] imetumika kuashiria silabi, wakati alama ya [#] inaonesha mwanzo na mwisho wa kitenzi kisoukomo.

3. Kanuni 1: Upachikaji wa Tonijuu Msingi (TJM) katika vitenzi visoukomo sahili vya Kirombo

Kanuni (1) inaeleza kuwa tonijuu msingi (TJM), inapaswa ipachikwe katika silabi ya kwanza ya shina katika vitenzi visoukomo vya Kirombo. Hivyo, kanuni inasomeka kuwa, kitenzi kinaweza kuwa na kiambishi awali (kisoukomo) (KA) ambacho hufuatiwa na shina la kitenzi kisoukomo sahili, ambapo TJM huhusishwa na silabi ya kwanza ya shina linalohusika. Tufafanue kidogo hasa tunaposema 'kitenzi kinaweza kuwa', hii ni kutokana na ukweli kuwa, katika lugha ya Kirombo, siyo kwamba vitenzi

vyote visoukomo vina toni J moja, vingi vina toni J zaidi ya moja ambavyo huanza na toni J kwenye silabi ya kwanza ya shina na kusambaa kuelekea kulia mwa shina ama hadi silabi ya mwisho kasoro mbili au moja kutoka mwishoni mwa shina la kitenzi hasa kwa vitenzi vya silabi tatu za shina hadi vile vyenye silabi sita za shina.




Kabla ya kuendelea na uchanganuzi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje la vitenzi visoukomo kwa kutumia kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina, ni vema tukaeleza kwamba, katika lugha ya Kirombo usoukomo huoneshwa kwa kutumia kiambishi awali [-i-]. Aidha, ni vema ikafahamika kuwa muundo wa vitenzi visoukomo sahili vya Kirombo huanza kwa Kiambishi awali (kisoukomo) [- i-] na kufuatiwa na shina la kitenzi husika [-shina]. Aghalabu kiambishi awali (kisoukomo) kimeonekana kuwa na tonichini hasa kinapoangaziwa katika muktadha wa kitoni.

### 5.1 Ujitokezaji wa Ruwaza za Toni katika Vitenzi Visoukomo Sahili vya Silabi Mbili za Shina.


Kutokana na matokeo ya utafiti, imegundulika kuwa vitenzi visoukomo sahili vya silabi mbili za shina vipo katika makundi mawili ambayo hutofautiana katika ruwaza za ujitokezaji wa toni katika vitenzi husika. Makundi hayo ni CJC na CSC. Kutokana na tofauti hizo za ujitokezaji wa ruwaza za toni katika makundi hayo, imesababisha maana ya vitenzi hivyo kubadilika.

Aidha, kwa kuanza na kundi la kwanza la vitenzi visoukomo sahili vya silabi mbili za shina, kama mifano yake inavyoonekana katika (5), ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika vitenzi hivyo imeonekana, kuanza na tonichini katika kiambishi awali (kisoukomo), kisha kufuatiwa na tonijuu katika silabi ya kwanza ya shina na tonichini katika silabi ya mwisho ya shina (CJC). Tuchunguze kwa makini mifano ya data ya kundi hili la vitenzi vya silabi mbili za shina.

5. a) i fé sa — ‘kuambia’
   b) i bá sha — ‘kuchonga’
   c) i kó rya — ‘kupika’
   d) i fé ya — ‘kukatia mbuzi’
   e) i bá rya — ‘kupasua kuni’

Tukitazama data (5) kitoni tunaweza kuona kuwa, vitenzi vyote vimeanza na tonichini, ikifuatiwa na tonijuu na kuishia na tonichini. Hivyo, kuwa na ruwaza ya ujitokezaji wa toni wa CJC. Hii ikiwa na maana kwamba, kiambishi awali / i- / ambacho ni kisoukomo cha vitenzi visoukomo vya Kirombo kina toni C, ambayo hufuatiwa na toni J ya silabi ya kwanza ya shina na silabi zote za mwisho wa shina la kitenzi kisoukomo kimebeba toni C. Ukokotozi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani umefanyika kwa kuzingatia kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina la kitenzi kisoukomo. Baada ya upachikaji wa TJM katika vitenzi hivi vya silabi mbili bado hatupati umbo la toni linalokubalika katika kirombo kwa sababu kuna vitamkwa ambavyo vinakuwa havina toni yaani [ø]. Ni vizuri ikumbukwe kwamba katika taaluma ya toni, haina maana ya kuwa ni toni chini. Hivyo ili kuwa na matokeo sahihi ya toni, kama ilivyo katika lugha nyingine zinazochanganuliwa toni, ipo haja ya kuwa na kanuni ya toni itakayozingatia na kuhusisha vitamkwa vyote vilivyo na [ø] na toni juu, kuvihusisha na toni chini. Hivyo kanuni inayohusika ni uhusishaji toni chini kwa vitamkwa visivyo na toni, na ambayo tunaweza kuichonga kama ifuatavyo:

Kanuni 4; uhusishaji wa Kitamkwa na Toni chini:




Kanuni hii inasomeka kuwa, irabu isiyo na toni ihusishwe na toni chini.

Baada ya uundaji wa kanuni ya uhusishaji wa irabu isiyo na toni, sasa tunaweza kutumia kanuni hiyo pamoja na kanuni nyingine ikiwemo kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina kukokotoa vitenzi vya silabi mbili hadi vile vyenye silabi sita za shina.

Hebu tuchunguze mfano wa ukokotozi katika 3 hapa chini, kwa kitenzi **i fé sa** ‘Kuambia’ itakuwa kama ifuatavyo:

/ i fe sa/ — ‘Umbo la ndani’
J
|
3. i fe sa — ‘Upachikaji wa TJM’
C J C
| | |
i fe sa — ‘Uhusishaji wa tonichini na Vitamkwa’
[ i fé sa ] — ‘Umbo la nje’

Ukokotozi wa (6) hapo juu umetupatia matokeo yanayokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo [ *i fé sa* ]. Matokeo haya yanaonesha kwamba, ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika kitenzi [ i fé sa ], huanza kwa toni C katika KA, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina kisha kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la kitenzi [ i fé sa ]. Aidha, katika ukokotozi wa (6) upangilifu wa kanuni umeanza kwa kutumia kanuni ya 1 ya upachikaji wa TJM tuliyoiunda hapo juu. Kanuni hiyo inaeleza kuwa, TJM inapaswa ihusishwe na silabi ya kwanza ya shina katika vitenzi visoukomo vya Kirombo. Kwa hali hiyo, mchakato wa ukokotozi wa umbo la nje katika vitenzi visoukomo sahili vya silabi mbili, umeanza kwa hatua ya kupachika TJM kwenye silabi ya kwanza ya shina, ikifuatiwa na uhusishaji wa tonichini (C) na vitamkwa. Hata hivyo, kama inavyoonekana katika (6) hatuhitaji kutekeleza hatua ya Sharti la Ukubalifu kwa sababu tayari limetimizwa katika kanuni ya pili ya uhusishaji wa tonichini na vitamkwa.

Matokeo haya yanashadidiwa na matokeo ya tafiti nyingine za lugha za Kibantu kama vile: utafiti aliofanywa na Hyman (2017:86) katika uhakiki wa toni za Kibantu ambapo aligundua kwamba vitenzi visoukomo sahili vya silabi mbili za shina katika Kihaya vina ruwaza ya ujitokezaji wa toni kwa kuanza na toni C, ikifuatiwa na toni J kisha toni C katika silabi ya mwisho ya shina kama vile inavyoonekana katika kitenzi [*ku-bó-na]* ‘kuona’. Pia, Marlo (2013:97) alibainisha kuwa, vitenzi visoukomo vya silabi mbili za shina katika Kiluyia vina ruwaza ya utokeaji wa toni unaoanza na

toni C katika kiambishi awali kisoukomo /ʊ̀/, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina kama mifano ya vitenzi hivyo inavyoonekana katika:

. a) ʊ̀[rá-a] 'to sleep' kulala (tafsiri yangu)
b) ʊ̀[xá-na] 'to deny' kukataa (tafsiri yangu)

Hata hivyo, kunaweza kuwa na utofauti wa ujitokezaji wa ruwaza ya toni katika vitenzi visoukomo sahili vya Kibantu. Kwa mfano ruwaza ya vitenzi visoukomo sahili katika Kiganda inaweza kuanza kwa toni kati (-) katika kiambishi awali kisoukomo, kisha kufuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina kama inavyoonekana katika kitenzi [ā-bón-a] (Myers, 1998: 87). Pamoja na utofauti huo wa ruwaza ya ujitokezaji wa toni bado haijabadilisha toni juu kuhusishwa na silabi ya kwanza ya shina la kitenzi kisoukomo sahili. Kwa hali hiyo, hatuna budi kuendelea na kundi la pili la vitenzi visoukomo sahili vya silabi mbili za shina.

Aidha, kundi la pili (CSC) la vitenzi visoukomo sahili vya silabi mbili kama ilivyobainika katika matokeo ya utafiti huu vimeonekana kuwa, ujitokezaji wa ruwaza za toni huanza na toni C, kisha kufuatiwa na tonishuka (TS) na kuishia mwisho na toni C. Tuchunguze mifano ya vitenzi visoukomo sahili vya kundi hili katika jedwali la 7 hapa chini:

**Jedwali la 1:** Nafasi ya Tonijuu dhidi ya Tonishuka

| Na. | A: (J) | Maana | B: (TS) | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 1. | i tó la | Kuruka | i tô la | Kudonoa, |
| 2. | i fí na | Kutoa | i fî na | Kuimba |
| 3. | i lá rya | Kuvaa | i lâ rya | Kulaza |
| 4. | i á la | Zuia | i â la | Kutandika |
| 5. | i mwí ra | Kukamata | i mwî ra | Kubeba |
| 6. | i sú fa | Kukuna | i sû fa | Kuchukia |
| 7. | i sá na | kuhasi (mbuzi) | i sâ na | Kuokota |
| 8. | i kó rwa | Kuchoma | i kô rwa | Kukooa |
| 9. | i fí shya | Kutema | i fî shya | Kulisha kwa mdomo |
| 10. | i ú mya | Kusindikiza | i û mya | Kuumia |
| 11. | i fí a | Kupaka | i fî a | Kutoa jasho |


Kutokana na data ya jedwali (1) hapo juu, tumebaini kuwa orodha ya vitenzi visoukomo sahili vya silabi mbili vina kiambishi kisoukomo / i- / katika safu zote, yaani **A** na **B** kimebeba toni C na silabi zote za mwisho wa shina katika safu zote zimebeba pia toni C. Aidha, tumebaini kuwa, vitenzi visoukomo sahili vilivyopo katika safu **A** na **B** vina idadi sawa ya silabi na zinazofanana kimofolojia. Aidha, tofauti ya vitenzi visoukomo sahili vilivyopo katika safu hizo mbili hutokana na ukweli kwamba, vitenzi visoukomo sahili katika safu **A,** vina toni J katika silabi ya kwanza ya shina, ilhali vilivyopo katika safu **B** vina toni TS katika silabi ileile ya kwanza ya shina. Yaani, ukitazama kwa makini katika data ya jedwali la 7 utagundua kwamba silabi zilizopigiwa msitari katika safu **B** zote zimebeba toni TS, wakati silabi hizo hizo katika safu **A** zimebeba toni J. hii inatokana na ukweli kwamba utamkaji wowote hutegemea kusudi la usemaji ambao hutofautishwa kwa uwekaji wa toni tofauti katika nafasi ileile ya utokeaji wa toni nyingine. Hali hii hufanya ujitokezaji wa ruwaza ya toni katika vitenzi visoukomo sahili kutofautiana na hivyo kuleteleza tofauti za kimaana.

Hutokeaji wa toni katika kundi la pili ni tofauti kabisa na kundi la kwanza, hali iliyotulazimu tuifafanue lau kwa ufupi kabla ya kuendelea na ukokotozi wetu. Aidha, Katika kundi hili tonishuka (TS) hujitokeza kwenye nafasi ya TJM, hali ambayo ni tofauti na kundi la kwanza. Hali hii imetufanya tuhitajie kufahamu mambo yafuatayo: moja, tumehitaji kufahamu sababu zilizofanya TS ijitokeze katika nafasi ya TJM. Mbili, tumehitaji kufahamu TJM inapachikwa wapi na kwa nini imebadilika? Na jambo la tatu ni kuwa, tumehitaji kufahamu kanuni na michakato iliyosababisha ujitokezaji wa TS hadi kuleteleza kubadilika kwa maana ni ipi? Kabla ya kukokotoa data ya kundi la pili katika safu **B** ni vema kutoa maelezo yaliyotuwezesha kupata majibu ya maswali tuliyojiuliza na ambayo yamekuwa ni dira ya ukokotozi wa TS katika data ya safu **B** kwenye jedwali la 1.

Kuna wataalamu kama vile Goldsmith, (1976: 221; Snider, 1999:57; Hyman, 2007:2 na Massamba, 2011: 171 - 178) ambao kwa kutumia Nadharia ya FVH, wameonesha namna ya kukabiliana na changamoto za uchanganuzi wa TS kwa kupendekeza njia mbili mwafaka kutegemeana na lugha husika; Moja, walipendekeza kuwa, TS inapaswa kuchukuliwa kuwa ni toni huru kama zilivyo C na J na mbili, ni kuwa TS ni matokeo ya muunganiko wa toni J na C. Yaani, utamkaji wa silabi inayohusishwa na TS huwa na msikiko ambao huanzia juu na kushuka chini.

Kutokana na maelezo ya wataalamu hao, katika lugha ya Kirombo tunapendekeza ukokotozi wa TS uzingatie njia ya pili inayosema kuwa, TS ni matokeo ya muunganiko wa J na C baada ya kufanyika kwa mchakato wa kimofofonolojia wa udondoshaji wa kitamkwa fulani katika mazingira ya shada la irabu. Kulingana na Kiunzi cha Fonolojia Vipandesauti Huru, kinadai kuwa, kitamkwa kikidondoshwa, toni iliyokuwa ikihusishwa nayo uhamia katika toni jirani kwa kutumia kanuni ya ujirani (§. Hyman, 1978:259; Cassimjee, 1986:15 na Massamba, 2011: 175). Kanuni ya Ujirani inasema kwamba, toni fulani husababisha mabadiliko katika toni iliyo jirani yake. Yaani, inayotangulia ujulikana kama toni chombeza na inayofuatia ujulikana kama toni chombezwa. Hivyo, kulingana na kanuni ya ujirani, toni inayochombezwa sharti iwe jirani kabisa na toni inayochombeza. Katika lugha ya Kirombo kanuni ya ujirani hufanya kazi hasa kwenye shada la irabu, ambapo irabu moja udondoshwa wakati wa utamkaji na kuacha toni yake ikielea. Kwa mujibu wa Moller (2014) neno linaweza kusitiri toni msingi bila kuhihusisha na silabi. Ikitokea hivyo, neno husika litakuwa na toni inayoelea. Wakati wa utamkaji toni ya irabu iliyotangulia husababisha mabadiliko katika toni ya irabu inayoifuatia kwa kuifanya iungane kuwa toni moja ambayo msikiko wa utamkaji hauelekei tena juu na badala yake huwa na msikiko unaokwenda chini. Hata hivyo, utekelezaji wa kanuni ya ujirani hufanywa baada ya Sheria ya Upangiliaji kutekelezwa (§. Massamba, 2011: 192) kwa maelezo zaidi.

Kanuni 5: Ujirani wa Toni




Kanuni ya 2 ya ujirani wa toni inasema kuwa toni chombeza na chombezwa sharti ziwe zinafuatana. Katika kanuni hii toni chombeza ni toni J na toni chombezwa ni toni C. Ukichunguza kwa makini kanuni hii utagundua kwamba mwanzoni kila toni

imehusishwa na kitamkwa kimoja, baadae kulingana na michakato ya kifonolojia na kimofolojia kitamkwa cha pili kutoka mwishoni mwa shina kikadondoshwa na kuacha toni iliyohusishwa nacho kuelea. Hii ni kwa sababu katika mtazamo wa FVH toni si kiambajengo cha kitamkwa kilichotoweka. Kwa hiyo toni hubakia kwenye rusu yake. Hii inaonesha dhahiri kwamba vitamkwa na vipambasauti ni vipengele ambavyo vinajitegemea, kila kimoja kikiwa na rusu yake (Massamba, 2011:181). Kutokana na ueleaji huo wa toni na tukizingatia kanuni ya Sharti la Ukubalifu katika FVH, toni J ambayo ndiyo iliyotangulia na kufuatiwa na toni C inayoelea uungana na kuwa toni TS kutokana na ujirani wake.

Sasa tunaweza kutumia kanuni ya 2 ya ujirani wa toni tuliyoichonga hapo juu kukokotoa mifano ya vitenzi visoukomo sahili vilivyopo katika safu B kwenye jedwali la 1 kama ifuatavyo:

**itôla** **'Kudonoa'**

/i to la/ 'Umbo la ndani'

C J CC

8. i too la 'Kuhusisha toni na vitamkwa'

C J C C

i too la 'Udondoshaji wa kitamkwa [o]'

C J CC

i to la 'Kanuni ya ujirani'

CS C

i to la 'Sharti la Ukubalifu'

[i tô la ] 'Umbo la nje'

Ukokotozi wa (8) umetupatia matokeo yanayokubalika katika usemaji wa Kirombo [i tô la]. Matokeo ya ukokotozi (8) yanaonesha kwamba, ruwaza ya ujitokezaji wa toni huanza kwa toni C katika kiambishi awali, ikifuatiwa na toni TS katika silabi ya kwanza ya shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina. Hata hivyo, matokeo haya hayakinzani na matokeo ya utafiti wa vitenzi vya silabi mbili za shina Kihaya kama vile [ku-bôn-a] 'kuona' (Hyman na Byarushengo, 1984:86). Katika ukokotozi (8) inaonekana kwamba uibuzi wake umepitia hatua nne tofauti. Hatua ya kwanza ni uhusishaji wa toni na vitamkwa ambapo kila kitamkwa kimehusishwa na ama tonichini au tonijuu. Hatua hii imetangulia kulingana na Sheria ya Upangiliaji wa toni inayosema huwezi kudondosha toni kabla hujahihusisha na silabi maalumu na kinyume chake ni sahihi (Massamba, 2011: 192). Hatua ya pili imetekeleza sheria ya udondoshaji wa irabu [o] kabla ya kanuni ya ujirani kutekelezwa. Kanuni ya ujirani imetekelezwa katika hatua ya tatu na hivyo kutupa matokeo yanayokubalika [ *i tô la* ] katika lugha ya Kirombo.

## 5.2 Ujitokezaji wa Ruwaza za Toni katika Vitenzi Visoukomo Sahili vya Silabi Tatu za Shina


Baada ya kuona ruwaza za ujitokezaji wa toni katika vitenzi visoukomo sahili vya silabi mbili, sasa hatuna budi kuendelea na ukokotozi wa uibuzi wa toni katika vitenzi visoukomo sahili vya silabi tatu za shina la kitenzi. Katika Kirombo, ujitokezaji wa ruwaza za toni katika aina hii ya vitenzi vya silabi tatu ni wa CJJC. Tuchunguze data katika mfano wa (9):

9. a) itéréfa 'kuomba'
b) ibóryómwa 'kubomoa'
c) ikámáta 'kupeleka'
d) iámbúsa 'kupanguza'
e) ilúngána 'kufuatana'

Ukichunguza kwa makini data ya 9 (a – e) hapo juu, utagundua kwamba, vitenzi visoukomo sahili vilivyopo vina idadi sawa ya silabi tatu za shina la kitenzi. Pia, vyote vimeanza kwa kiambishi kisoukomo /i/. Alkadhalika, utagundua kuwa, vitenzi visoukomo sahili vyote katika data hii vina toni J mbili ambazo hujitokeza katika silabi ya kwanza ya shina hadi silabi ya pili ya shina la vitenzi husika. Sanjari na hayo, utagundua kuwa, kiambishi kisoukomo cha vitenzi visoukomo sahili vya Kirombo na silabi ya mwisho ya shina katika data (9) hapo juu zote zina toni C. Hivyo, kutokana na data (9) utagundua kwamba, ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika vitenzi hivyo ni CJJC. Yaani, vitenzi vyote vimeanza na toni C katika kiambishi kisoukomo, na tonijuu mbili zinazofuatana katika shina la kitenzi na kufuatiwa toni C katika silabi ya mwisho ya shina. Swali tunalojiuliza kutokana na data ya (9) hapo juu ni kwamba, kwa nini ina toni J mbili?, Je, toni J mbili zinazoandamana katika silabi za mashina ya hivyo vitenzi visoukomo sahili ni ujirudiaji wa toni J? Na je, mojawapo ya toni J hizo inaweza kudondoshwa? Je, ikidondoshwa madhara yake kitoni ni yepi?

Aidha, ukweli tulioubaini katika data (9) ni kwamba, hakuna TJM mbili, bali kuna ujirudiaji wa toni J ya silabi ya kwanza ya shina unaojitokeza kuelekea kulia mwa shina la kitenzi. Kwa hali hiyo, udondoshaji wa TJM ya shina hujitokeza ili kuondoa dhana ya kuwa na TJM mbili katika silabi za shina moja zinazofuatana na hivyo kuruhusu toni J ya kwanza ya shina ijirudie katika silabi ya pili ya shina. Hali ya ujirudiaji wa toni kuelekea kulia au kushoto mwa shina kitoni huitwa *msambao wa toni*. Hivyo, toni J ya silabi ya kwanza ya shina husambaa kuelekea kulia mwa shina la kitenzi na siyo kwamba ni toni J mbili tofauti. Kutokana na ujidhihirishaji wa ruwaza ya msambao wa toni J, tuliona kuna haja ya kuunda kanuni iliyotusadia katika ukokotozi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la vitenzi visoukomo sahili vya silabi tatu za shina kama inavyoonekana katika kanuni (18) hapa chini:

6. Kanuni ya 6: Msambao wa Tonijuu




Kanuni (6) inasomeka kuwa, tonijuu inasambaa kuelekea kulia mwa shina la kitenzi, ikiwa na maana kuwa tonijuu huanzia silabi ya kwanza ya shina hadi ama silabi ya mwisho kasoro mbili au moja kutoka mwishoni mwa kitenzi kisoukomo sahili.

Kutokana na kanuni (6) tunaweza kukokotoa vitenzi visoukomo sahili vya silabi tatu za shina vilivyopo katika data (9) kwa kutumia mfano wa kitenzi kisoukomo /i te re fa/ 'kuomba' hapo juu, kama ifuatavyo:

i té ré fa 'Kuomba'

/i te re fa/ 'Umbo la ndani'

J

9. i te re fa 'Upachika wa TJM'

J

i te re fa 'Usambaaji wa Tonijuu'

C J C

i te re fa 'Uhusishaji Tonichini na Vitamkwa'

C J J C

i te re fa 'Sharti la Ukubalifu'

[i té ré fa] 'Umbo la nje'

Ukokotozi wa mfano (9) hapo juu, umetupatia matokeo yanayokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kirombo [i té ré fa]. Matokeo haya yanaonesha kwamba kiambishi kisoukomo /i/ kina toni C ambayo hufuatiwa na toni J ya silabia ya kwanza ya shina na ambayo usambaa hadi silabi ya mwisho kasoro moja kutoka mwishoni mwa shina la kitenzi / i te re fa/ na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina. Aidha, ukichunguza kwa makini ukokotozi wa mfano wa (9) utagundua kwamba, kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina la kitenzi kisoukomo sahili imetekelezwa katika hatua ya mwanzo kabisa. Pia, kanuni (6) ya usambaaji wa toni J kuelekea kulia mwa shina katika ukokotozi wa mfano (9), imetekelezwa kabla ya utekelezaji wa hatua ya uhusishaji wa Tonichini na vitamkwa. Sanjari na hayo, kanuni ya Sharti la Ukubali imetekelezwa katika hatua ya mwisho ya ukokotozi huu. Hivyo, kulingana na matokeo ya ukokotozi huu na utaratibu wa utumiaji wa kanuni ya usambaaji wa toni J uliotumika, ukokotozi huu umetupatia matokeo yanayokubalika katika lugha ya Kirombo. Kwa hali hiyo, hatuna budi kuendelea na ukokotozi wa vitenzi visoukomo sahili vya silabi nne kama ifuatavyo:

### 5.3 Ujitokezaji wa Ruwaza za Toni katika Vitenzi Visoukomo Sahili vya Silabi Nne za Shina

Katika 5.2 tumejadili kwa kina na tumeona ruwaza za ujitokezaji wa toni katika vitenzi visoukomo sahili vya silabi tatu za shina. Aidha, tumeona namna kanuni (6) ya usambaaji wa toni J kuelekea kulia mwa shina la kitenzi inavyofanya kazi katika ukokotoaji wa hivyo vitenzi visoukomo sahili vya silabi tatu za shina. Katika sehemu hii tumeendelea na ukokotozi wa vitenzi visoukomo sahili vya silabi nne za shina katika kuibua toni kwenye umbo la nje kutoka umbo la ndani la vitenzi husika. Utafiti umebaini kuwa, ujitokezaji wa ruwaza za toni katika aina hii ya vitenzi visoukomo sahili vya silabi nne za shina upo katika makundi matatu ambayo ni CJJJC, CJJCC na CCJJC Tuchunguze data (10) hapa chini:

Tuanze kujadili makundi hayo matatu ya vitenzi visoukomo sahili vya silabi nne za shina kwa kuanza na kundi la kwanza katika 10(a-e), kundi hilo lina ruwaza ya ujitokezaji wa toni wa CJJJC. Chunguza data 10(a-e) hapa chini:

10. a) ibéryéngésa 'kukalia kitu kisicho mororo'
b) ilémbéryána 'kusingiziana'
c) idólyíryána 'kupandishiana'
d) iséngéryána 'kuchekeshana'
e) itámbúkyána 'kutembeleana'

Kundi hili kimofolojia limeundwa kwa silabi nne za shina. Vitenzi visoukomo vyote katika 10(a-e) vina kiambishi awali /i-/ ambacho pia, ni kisoukomo cha vitenzi visoukomo vya Kirombo. Hapa yafaa ieleweke kwamba si kila kiyeyusho kilichopo katika silabi huwa kimetokana na mchakato wa uyeyushaji katika Kirombo. Kwa mfano, viyeyusho vilivyopo katika vitenzi visoukomo sahili kama vile: *iséngéryána*, *ibéryéngésa* na *itíngílyao* havijatokana na mchakato wa uyeyushaji bali katika Kirombo huchukuliwa kama sauti moja inayojitegemea. Kitoni, katika data 10(a-e) kiambishi kisoukomo /i-/ kina toni C, inayofuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na ambayo pia usambaa kuelekea kulia mwa shina hadi silabi ya mwisho kasoro moja kutoka mwishoni mwa shina la vitenzi visoukomo sahili husika na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina. Kwa kuwa data hii ina msambao wa toni J kama ilivyokuwa katika 4.3.2, kanuni (6) ya msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina la kitenzi iliyotumika kukokotolea data (9) katika mifano ya (9) unavyoonekana hapa chini:

**ibéryéngésa** **'Kukalia kitu kisicho mororo'**

/i be rye nge sa/ 'Umbo la ndani'

J

10. i be rye nge sa 'Upachikaji wa TJM'

J

i be rye nge sa 'Usambaaji wa Tonijuu'

C J C

i be rye nge sa 'Uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa'

C J J J C

i be rye nge sa 'Sharti la Ukubalifu'

[i bé ryé ngé sa] 'Umbo la nje'

Ukokotozi wa mfano (10) hapo juu, umetupatia matokeo yanayokubalika katika usemaji wa Kirombo [i bé ryé ngé sa]. Ukichunguza kwa makini matokeo ya ukokotozi huu utagundua kwamba, kiambishi kisoukomo /i-/ na silabi ya mwisho ya shina la kitenzi kisoukomo sahili [i bé ryé ngé sa] vyote vimebeba toni C. Pia, matokeo yanaonesha kuwa, silabi ya kwanza ya shina imebeba toni J ambayo usambaa kuelekea kulia mwa shina hadi silabi ya

mwisho kasoro moja. Aidha, katika ukokotozi huu kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina imetekelezwa katika hatua ya mwanzo. Sanjari na hilo, kanuni ya msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina la kitenzi kisoukomo sahili [i bé ryé ngé sa], imetekelezwa kabla ya utekelezaji wa hatua ya uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa. Pia, hatua ya Sharti la Ukubalifu limetekelezwa katika hatua ya mwisho katika ukokotozi wa uibuzi wa umbo la nje kutoka umbo la ndani la kitenzi kisoukomo sahili [i bé ryé ngé sa]. Tunaweza kuendelea na ukokotozi wa kundi la pili la vitenzi visoukomo sahili vya silabi nne za shina vyenye ruwaza ya ujitokezaji wa toni wa CJJCC. Chunguza data ya 10(f – j) hapa chini:

| | | |
|---|---|---|
| 10. | f) ikándíkyao | 'Kusiribia hapo' |
| | g) ikíshíkyao | 'kufunikia hapo' |
| | h) itíngílyao | 'Kuchechemea hapo' |
| | i) iféníyílyao | 'Kumenyea hapo' |
| | j) iféshíryao | 'Kunong'onezea hapo |

kimofolojia data 10(f – j) hapo juu, imeundwa kwa silabi nne za shina na kiambishi awali /i-/ ambacho pia ni kisoukomo cha vitenzi visoukomo sahili husika. Ukichunguza kwa makini utaguundua kwamba vitenzi visoukomo sahili vya silabi nne za shina katika kundi la 10(f – j) vina muundo wa I, KI, KKI, KI (silabi hii imetokana na mchakato wa uyeyushaji) na kuishia na I. Aidha, katika 10(f- J), kitoni inaonekana kuwa, kiambishi awali na kisoukomo cha vitenzi visoukomo vya Kirombo, kina toni C, ambayo hufuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na ambayo usambaa kuelekea kulia mwa shina la kitenzi kisoukomo hadi silabi ya mwisho kasoro mbili kutoka mwishoni mwa shina la vitenzi husika. Pia, silabi ya mwisho ya shina katika kundi la 10 (f – j) imebeba toni C. Hebu tuchunguze ukokotozi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la kitenzi kisoukomo sahili /ikandikyao/ '*Kusiribia hapo'* katika (11) hapa chini:

**ikándíkyao** **'Kusiribia hapo'**

/i ka ndi kya o/ 'Umbo la ndani'

J

11. i ka ndi kya o 'Upachikaji wa TJM'

J

i ka ndi kya o 'Msambao wa Tonijuu'

C J C

i ka ndi kya o 'Uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa'

C J J C C

i ka ndi kya o 'Sharti la Ukubalifu'

[i ká ndí kya o] 'Umbo la nje'

Katika ukokotozi (11) hapo juu, tumepata matokeo yanayokubalika katika useamji wa Kirombo [i ká ndí kya o]. Matokeo ya ukokotozi wa (11) yanaonesha kwamba, silabi mbili za mwisho wa shina zimebeba toni C. Pia, matokeo ya ukokotozi huu yanaonesha kuwa kiambishi kisoukomo na ambacho ni kiambishi awali cha kitenzi kisoukomo sahili [i ká ndí kya o] nacho kimebeba toni C. Sanjari na hayo, matokeo yanaonesha kuwa silabi ya kwanza ya shina imebeba toni J ambayo usambaa kuelekea kulia mwa shina hadi silabi ya pili ya shina. Matokeo ya ukokotoz wa (11) ndiyo yanayodhihirisha wazi kwamba, ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika 10(f-j) ambalo ni kundi la pili la vitenzi visoukomo sahili vya silabi nne za shina kuwa ni CJJCC. Aidha, katika ukokotozi (11), kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina la kitenzi kisoukomo sahili imetekelezwa katika hatua ya mwanzo. Pia, kanuni ya msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina imetekelezwa kabla ya utekelezaji wa hatua ya uhusishaji wa Tonichini na vitamkwa. Hatua ya Sharti la Ukubali imetekelezwa mwishoni katika ukokotozi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani katika (11) hapo juu.


Kutokana na matokeo ya kundi la kwanza 10(a-e) na la pili 10(f-j), hatuna budi kuendelea na ukokotozi wa kundi la tatu lenye ruwaza ya ujitokezaji wa toni wa CCJJC katika data 10(k- p). Chunguza kwa makini data ya 10(k-p) hapa chini:

| | | |
|---|---|---|
| 10. | k) iidikirya | 'kusalimia' |
| | m) iisakulya | 'kuangalia' |
| | n) iitukulya | 'kuona' |
| | o) iitanyana | 'kusikilizana' |
| | p) iirilyana | 'kushikiliana' |

Kimofolojia kundi la vitenzi visoukomo sahili katika 10(k-p) vina idadi ya silabi nne za shina na kiambishi awali /i-/ kama ilivyo kwa makundi yalikwishajadiliwa katika 10(a-e) na 10(f-j) hapo juu. Pia, kundi la tatu katika 10(k-p) mwishoni mwa shina uishilia na silabi yenye muundo wa KI ambazo ni mchanganyiko wa silabi zenye viyeyusho vilivyotokana na mchakato wa uyeyushaji kama ilivyofafanuniliwa katika 10(f-j). Kitoni, data 10(k-p) inaonekana kuwa na toni C katika kiambishi kisoukomo /i-/, ikifuatiwa na toni C katika silabi ya kwanza ya shina. Aidha, hufuatiwa na toni J katika silabi ya pili ya shina na ambayo usambaa kuelekea kulia hadi silabi ya mwisho kasoro moja kutoka mwishoni mwa shina. Aidha, silabi ya mwisho ya shina katika 10(k-p) ina toni C.

Katika kundi la tatu, hali ya ujitokezaji wa toni J katika silabi ya pili ya shina imetufanya tujiulize swali, Je, nini kilichosababisha toni J ianze kujitokeza katika silabi ya pili badala ya silabi ya kwanza ya shina kama ilivyokuwa kwa makundi mengine ya vitenzi visoukomo sahili yaliyotangulia? Jibu la swali hili ni kwamba, irabu /i/ ambayo ni silabi ya kwanza ya shina katika 10(k-p) ikitanguliwa na kiambishi awali /i-/ na ambacho ni kiambishi kisoukomo cha vitenzi visoukomo sahili vya Kirombo huathiriwa, na hivyo katika utamkwaji wake huwa na msikiko wa chini. Hivyo, ujitokezaji wa toni J katika silabi ya pili ya shina hutueleza kuwa, toni J imehama kutoka silabi ya kwanza ya shina kwenda silabi ya pili ya shina la vitenzi visoukomo katika 10(k-p). Ili kuweza kukabiliana na suala la uhamaji wa toni J tumehitajia kuunda kanuni ya *Uhamaji wa Tonijuu Msingi* iliyotumika katika ukokotozi wa kundi la tatu, kwani ni vigumu kukokotoa data ya kundi hili kwa kutumia kanuni nyingine, ikiwemo kanuni ya msambao wa toni J pekee. Tuchunguze kanuni (9) hapa chini:

**Kanuni ya 9: Uhamaji wa Tonijuu Msingi (TJM)**




Alama ya dola ($) katika kanuni ya 9 hapo juu ina maana ya silabi. Hivyo, kanuni ya 9 inasomeka kuwa, TJM ya silabi ya kwanza ya shina uhamia katika silabi ya pili ya shina la vitenzi visoukomo sahili vya silabi nne za shina vyene ruwaza inayoanza na ujitokezaji wa toni C katika silabi ya kwanza ya shina. Hebu tuchunguze mfano wa uchanganuzi katika (12) hapa chini:

| | | |
|---|---|---|
| | **i i mbí ryí sa** | **'Kubiringisha'** |
| | /i i mbi ryi sa/ | 'Umbo la ndani' |
| | J | |
| 12. | i i mbi ryi sa | 'Upachikaji wa TJM' |
| | J | |
| | i i mbi ryi sa | 'Uhamaji wa TJM' |
| | J | |
| | i i mbi ryi sa | 'Usambaaji wa Tonijuu' |
| | C J C | |
| | i i mbi ryi sa | 'Uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa' |
| | CC J J C | |
| | i i mbi ryi sa | 'Sharti la Ukubalifu' |
| | [ i i mbí ryí sa] | 'Umbo la nje' |

Katika (12) hapo juu, ukokotozi wake umetupatia matokeo yanayokubalika katika usemaji wa Kirombo [i i mbí ryí sa]. Matokeo ya (12) hapo juu yanatueleza kwamba, Kiambishi kisoukomo kimebeba toni C, ikifuatiwa na toni C katika silabi ya kwanza ya shina. Pia, matokeo ya ukokotozi wa (12) yanaonesha kwamba, silabi ya pili ya shina imebeba toni J ambayo pia usambaa kuelekea kulia hadi silabi ya mwisho kasoro moja kutoka mwishoni mwa shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la kitenzi kisoukomo sahili [i i mbí ryí sa]. Ukichunguza ukokotozi wa (12) utagundua kuwa, kuna uhamaji wa TJM kutoka silabi ya kwanza ya shina kwenda silabi ya pili ya shina. Katika Kirombo, kanuni ya uhamaji wa TJM hutekelezwa kabla ya kanuni ya msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina. Pia katika ukokotozi wa (12), hatua ya uhusishaji wa tonichini na vitamkwa imetekelezwa baada ya utekelezwaji wa kanuni ya msambao wa toni J na kabla ya utekelezwaji wa sharti la kubalifu. Utaratibu huu wa ukokotozi ni tofauti na mifano ya (10, na 11) ya kundi la kwanza na la pili katika vitenzi visoukomo sahili vya silabi nne za shina kwa sababu haijahusisha uhamaji wa toni J.

Uhamaji wa toni J kutoka silabi moja kwenda silabi nyingine katika shina katika matokeo ya ukokotozi (12) hushadidiwa na matokeo ya vitenzi visoukomo vya silabi nne za shina katika lugha nyingine za Kibantu kama vile: Kijita ambacho kinaonesha kuwa toni J inaweza kuhamia katika silabi ya pili ya shina kutoka silabi ya kwanza ya shina. Kwa mfano, katika kitenzi /ku-ßón-er-an-a/ kinaonekana kuwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina kabla ya uhamaji, ila ikihama uonekana katika silabi ya pili ya shina (a) [ku-ßon-ér-an-a] (Downing, 1990a) matokeo ya Downing katika Kijita huonekana kuwa sawa na yale ya kitenzi [*iitányána]* 'kusikilizana' cha Kirombo. Pia, Downing, (1990b:265) anaonesha Kizulu pia kina uhamaji wa toni J, ingawa uhamaji huo huonekana kuwa hauhamii kwenye silabi zinazofuatana katika shina, badala yake huruka baadhi ya silabi hata mbili katika shina. Kwa mfano:

b). /ú-ku-hlek-is-an-a/ → [u-ku-hlek-ís-an-a] 'kuchangia kila mmoja'.

Katika mfano (b) inaonekana kuwa kabla ya uhamaji toni J ipo katika kiambishi awali kitangulizi {u-, ila baada ya uhamaji toni J inaonekana katika silabi ya pili ya shina. Kirombo hakina hali ya uhamaji kama huu unaojitokeza katika Kizulu. Hata hivyo, kuna lugha nyingine za Kibantu zenye uhamaji wa toni J kutoka katika neno moja hadi neno jingine katika tungo. Kwa mfano, katika Kimijikenda kuna tungo /á-na-mal-a ku-gul-a ŋguwo/⟶ [a-na-mal-a ku-gul-a ŋguwó] yenye maana ya '*yeye anataka kununua nguo*'(Volk, 2011:54). Matokeo ya Volk yanaonesha kwamba, toni J imehamia katika silabi ya mwisho ya neno la tatu katika tungo kutoka katika Kiambishi awali [a].

### 5.4 Ujitokezaji wa Ruwaza za Toni katika Vitenzi Visoukomo Sahili vya Silabi Tano za Shina

Baada ya kujadili ruwaza za ujitokezaji wa toni katika vitenzi visoukomo sahili vya silabi nne, kwa kutalii makundi matatu ya CJJJC, CJJCC na CCJJC kama yalivyokwishafafanuliwa hatuna budi kuendelea kutalii vitenzi visoukomo vya silabi tano za shina ambavyo kulingana na data ya utafiti vimebainika kuwa na makundi mawaili ya ruwaza za ujitokezaji wa toni ambayo ni: CJJJJC na CJJCJC. Hebu tuchunguze data (13) hapa chini:

| | | |
|---|---|---|
| 13) | a) ifáfásíryána | 'kuelekezana' |
| | b) itétúkúlyána | 'kutoangaliana' |
| | c) imátíkílyána | 'kugongana mahali fulani' |
| | d) isúmánányándu | 'kukutana sehemu' |
| | e) isósófíkyána | 'kuchokozana' |
| | f) ifásíkányáse | 'kuwachongea tena' |
| | g) itámbílyatábu | 'kung'nga'nia' |
| | h) isúngúsyanáse | 'kutengenezeana tena' |
| | i) itóngóryanáse | 'kutembezana tena' |
| | j) idíshílyanáse | 'kukimbizana tena' |
| | k) ikúrýíkyanáse | 'kufichiana tena' |

Ukiichunguza kwa makini data (13) hapo juu, utagundua kwamba, ina makundi mawili ya ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika vitenzi visoukomo sahili vya silabi tano za shina ambayo ni CJJJJC katika 13(a- f) na CJJCJC katika 13(g-k). Katika data (13), vitenzi visoukomo sahili vyote vina idadi sawa ya silabi za shina ambazo ni

tano na kiambishi kisoukomo /i-/. Ukichunguza muundo wa vitenzi visoukomo sahili katika (13), utagundua kwamba, kundi la kwanza katika 13(a-f) lina kiyeyusho katika silabi ya mwisho kasoro moja wakati kundi la pili katika 26(g-k) lina konsonanti na irabu katika silabi ya mwisho kasoro moja. Pia, katika 13(a-f) kuna konsonanti na irabu kuanzia silabi ya kwanza ya shina hadi silabi ya tatu ya shina, wakati katika 13(g-k) kuna konsonanti na irabu katika silabi ya pili na kufuatiwa na konsonanti, konsonanti na irabu katika silabi ya pili hadi ya tatu ya shina.

Kitoni, katika 13(a-f) kiambishi kisoukomo kimebeba toni C, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina ambayo usambaa kuelekea kulia hadi silabi ya pili kasoro moja kutoka mwishoni mwa shina la kitenzi na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la vitenzi visoukomo sahili husika. Aidha, inaonekana dhahiri kuwa ruwaza ya ujitokezaji wa toni hubadilika kulingana na muundo wa aina ya kitenzi chenyewe kama inavyodhihirika katika 13(g-k) ambapo ruwaza ya ujitokezaji katika vitenzi vya data 13(g-k) ni CJJCJC, ambayo ni tofauti na ya kundi la kwanza. Yaani, katika kundi hili kiambishi kisoukomo kimebeba toni C, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na ambayo usambaa hadi silabi ya pili kutoka mwanzoni mwa kitenzi, kwa kutatizwa na ujitokezaji wa toni C, katika silabi ya tatu ya shina. Aidha, toni J hujitokeza tena katika silabi ya pili kasoro moja kutoka mwishoni mwa shina la kitenzi na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la vitenzi husika ambayo ni tabirifu. Tuchunguze mfano wa ukokotozi wa data ya kundi la kwanza kama inavyoonekana katika (13) hapa chini:

ifáfásíryána 'kuelekezana'

/ifafasiryana/ 'Umbo la ndani/

J

13. i fa fa si rya na 'Upachikaji wa TJM'

J

i fa fa si rya na 'Usambaaji wa Tonijuu'

C J C

i fa fa si rya na 'Uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa'

C J J J J C

i fa fa si rya na 'Sharti la Ukubalifu'


[i fá fá sí ryá na] 'Umbo la nje'

Ukokotozi wa (14) hapo juu, umetupatia matokeo yanayokubalika katika usemaji wa Kirombo [i fá fá sí ryá na]. Matokeo ya ukokotozi wa (14) yanaonesha kwamba, kiambishi kisoukomo /i-/ na silabi ya mwisho ya shina zote zimebeba toni C. Pia, silabi ya kwanza ya shina imebeba toni J ambayo pia usambaa kuelekea kulia hadi silabi ya mwisho kasoro moja. Aidha, ukichunguza kwa makini ukokotozi (14) utagundua kuwa kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina imetekelezwa katika hatua ya mwanzo ya ukokotozi. Pia, kanuni ya msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina, imetekelezwa kabla ya utekelezwaji wa hatua ya uhusishaji wa tonichini na vitamkwa. Kulingana na Nadharia ya FVH, hatua ya Sharti la Ukubalifu katika ukokotozi wa (14), limetekelezwa Katika hatua ya mwisho.

Baada ya kuona matokeo ya ukokotozi wa uibuzi wa toni katika kundi la kwanza la vitenzi visoukomo sahili vya silabi tano za shina, tunaweza kuendelea na ukokotozi wa kundi la pili la data 13(g-k) ambalo lina ruwaza ya ujitokezaji wa toni wa CJJCJC katika vitenzi visoukomo sahili vya silabi tano za shina la kitenzi. Hata hivyo, ukichunguza ruwaza ya data 13(g-k) ambayo ni CJJCJC, utagundua kwamba mwendelezo wa usambaaji wa toni J kutoka silabi ya kwanza kuelekea kulia mwa shina umezuiliwa kwa ujitokezaji wa toni C katikati ya shina na kisha kufuatiwa tena na toni J. Ujitokezaji wa toni C katikati hakuzuii msambao wa toni J kuelekea kulia pekee bali pia hufanya vitenzi visoukomo sahili katika 13(g-k) kuwa na TJM mbili. Hii ni kwa sababu toni C inapojitokeza katikati huanza ruwaza nyingine ambayo ufuatiwa na toni J nyingene kama vile mwanzoni mwa kitenzi na kuishia na toni C. Hali hii ya ujitokezaji wa TJM mbili katika kitenzi kimoja haiwezi kukokotolewa kwa kutumia kanuni ya msambao wa toni kuelekea kulia mwa shina pekee na kutupatia majibu yanayokubalika katika Kirombo kama mfano wa (14) unavyoonekana; **isúngúsyanáse 'kutengenezeana tena'** baada ya ukokotozi matokeo yake ni [*i sú ngú syá ná se] 'Umbo la nje'. Matokeo hayo hayakubaliki katika usemaji wa wazungumzaji wazawa wa Kirombo.

Ukichunguza data (14) kwa makini, utagundua kuwa kanuni ya msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina haiwezi kufanya kazi pekee, kwa sababu hiyo, tunapendekeza kanuni ya *Unakiliji wa TJM* itumike baada ya utekelezaji wa kanuni ya jumla ya Upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina kabla ya kutekelezwa kwa kanuni ya msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina la vitenzi visoukomo sahili vya shilabi tano za shina katika Kirombo. Chunguza kanuni ya Unakiliji wa TJM katika silabi ya nne ya shina hapa chini:

10. Kanuni ya 10. Unakiliji wa TJM




Katika kanuni ya 10 hapo juu, alama ya ($) iliyotumika ina maana ya silabi. Hivyo, kanuni ya 10 inasomeka kuwa, nakilisha TJM katika silabi ya nne ya shina kutoka silabi ya kwanza ya shina katika vitenzi visoukomo sahili vya silabi tano za shina, vyenye C katika silabi ya tatu kasoro mbili kutoka mwishoni mwa shina la vitenzi husika. Hebu tuchunguze mfano (15) wa ukokotozi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la vitenzi vya kundi la pili katika 13(g-k) kwa kutumia kanuni ya 10 katika (13) hapa chini:

**isúngúsyanáse** **'kutengenezeana tena'**

/isungusyanase/ 'Umbo la ndani'

J

13. i su ngu sya na se ‘Upachikaji wa TJM’

J

i su ngu sya na se ‘Unakiliji wa TJM’

J J

i su ngu sya na se ‘Usambaaji wa Tonijuu’

C J C J C

i su ngu sya na se ‘Uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa’

C J J C J C

i su ngu sya na se ‘Sharti la Ukubalifu’

[I sú ngú sya ná se] ‘Umbo la nje’

Katika ukokotozi wa (13) hapo juu, umetupatia matokeo yanayokubalika katika usemaji wa Kirombo [*i sú ngú sya ná se*]. Matokeo ya ukokotozi wa (13) hapo juu yanaonesha kuwa ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika kitenzi kisoukomo sahili [i sú ngú sya ná se], huanza kwa toni C katika kiambishi kisoukomo /i-/ ambacho pia ni kiambishi awali, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na ambayo usambaaa kuelekea kulia mwa shina hadi silabi ya pili ya shina, kisha kufuatiwa na toni C katika silabi ya tatu ya shina ambayo hufuatiwa na toni J tena katika silabi ya nne ya shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la kitenzi. Katika matokeo (13), utagundua kwamba silabi ya tatu ya shina la kitenzi kisoukomo sahili [*i sú ngú sya ná se*] kwa sasa ina toni C tofauti na matokeo ya ukokotozi ambao ulionesha silabi hiyo ina toni J hali iliyoleteleza matokeo yasiyokubalika katika usemaji wa Kirombo [**i sú ngú syá ná se*]. Aidha, ukichunguza kwa makini katika ukokotozi (13) hapo juu, utagundua kuwa, kanuni ya jumla ya Upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina imetekelezwa katika hatua ya mwanzo ya ukokotozi. Pia, katika ukokotozi wa (13), kanuni ya unakilishaji wa TJM katika silabi ya nne ya shina imetekelezwa kabla ya utekelezwaji wa kanuni ya msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina na ambayo imefuatiwa na hatua ya uhusishaji wa tonichini na vitamkwa. Kulingana na Nadharia ya FVH sharti la ukubalifu limetekelezwa katika hatua ya mwisho ya ukokotozi wa kitenzi kisoukomo sahili [i sú ngú sya ná se]. Tunaweza kuendelea na ukokotozi wa ngazi nyingene ya vitenzi visoukomo sahili vya silabi sita za shina kama ifuatavyo:

### 5.5 Ujitokezaji wa Ruwaza za Toni katika Vitenzi Visoukomo Sahili vya Silabi Sita za Shina

Baada ya kujadili kwa kina ruwaza za ujitokezaji wa toni katika vitenzi visoukomo sahili vya silabi tano za shina la kitenzi kwa kutumia kanuni ya unakiliji wa TJM na msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina la kitenzi na kanuni nyingine zilizozingatiwa katika uchanganuzi wa uibuzi wa toni kutoka umbo la ndani kwenda umbo la nje, tunaweza sasa kutalii ruwaza ya toni katika vitenzi visoukomo sahili vya silabi sita za shina. Kulingana na data ya utafiti, imebainika kuwa ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika vitenzi visoukomo sahili vya silabi sita za shina hujitokeza kama vile: CJJJCJC. Chunguza data 15 hapa chini:

15. a) idíshílyánaséo ‘kukimbizana tena hapo’
b) ibáryílyánaséo ‘kupasuliana tena hapo’
c) ikúshúryánaséo ‘kukumbatiana tena hapo’
d) isúngúsyánaryéo ‘kutengenezeana hapo’
e) isóryómólyanáse ‘kuchomoleana tena’

Ukichunguza kwa makini data 15 hapo juu utagundua kwamba, kimofolojia vitenzi visoukomo sahili vyote vilivyopo vina silabi sita za shina ambazo zinalandana kwa namna moja au nyingine kimuundo na vyote vimeanza kwa kiambishi awali /i-/ ambacho pia ni kisoukomo cha vitenzi visoukomo vya Kirombo. Aidha, kitoni, vitenzi visoukomo vyote vina toni J nne katika silabi za shina na vina toni C mbili za shina na toni C moja ya KA. Pia, ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika vitenzi visoukomo sahili vya silabi sita za shina katika data ya 15 hapo juu imeanza kwa toni C katika kiambishi kisoukomo /i-/, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na ambayo usambaa kuelekea kulia mwa shina hadi silabi ya tatu ya shina, kisha kufuatiwa na toni C ambayo ujitokeza katikati katika silabi ya nne ya shina. Hii nayo hufuatiwa na toni J katika silabi ya tano ya shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la vitenzi husika.

Pia, ukichunguza kwa makini ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika 15 ambayo ni CJJJCJC utagundua kwamba ina TJM mbili kama ilivyokuwa kwa vitenzi vya silabi tano za shina katika data 10(g-k) ambayo tulilazimika kuiundia kanuni ya 10 ya unakiliji wa TJM. Kwa kuwa data ya 15 nayo ina TJM mbili, basi kanuni ya 10 ya unakiliji wa TJM imetumika katika ukokotozi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani katika 15 hapa chini:

**idíshílyánaséo** **‘Kukimbizana tena hapo’**
/i di shi lya na se o/ ‘Umbo la ndani’

J

15. i di shi lya na se o ‘Upachikaji wa TJM’

J

i di shi lya na se o ‘Unakiliji wa TJM’

J J

i di shi lya na se o ‘Usambaaji wa Tonijuu’

C J C J C

i di shi lya na se o ‘Uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa’

C J J J C J C

i di shi lya na se o ‘Sharti la Ukubalifu’

[i dí shí lyá na sé o] ‘Umbo la nje’

Katika ukokotozi wa (15) hapo juu, tumepata matokeo yanyokubalika katika usemaji wa Kirombo. Matokeo ya ukokotozi wa 15 hapo juu yanaonesha kuwa, ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika kitenzi kisoukomo sahili [i dí shí lyá na sé o], huanza kwa toni C katika kiambishi kisoukomo, ikifuatiwa na toni J katika silabi

ya kwanza ya shina na ambayo usambaa kuelekea kulia mwa shina hadi silabi ya tatu ya shina, kisha kufuatiwa na toni C, ambayo ujitokeza katikati katika silabi ya nne ya shina na ambayo hufuatiwa na toni J katika silabi ya tano ya shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la vitenzi husika. Pia, ukichunguza kwa makini ukokotozi wa 15, utagundua kwamba kanuni ya jumla ya Upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina imetekelezwa katika hatua ya mwanzo ya uchanganuzi. Pia, Kanuni ya unakiliji wa TJM ambayo imenakilishiwa katika silabi ya tano ya shina, imetekelezwa kabla ya utekelezwaji wa kanuni ya msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina na kufuatiwa na utekelezaji wa hatua ya uhusishaji wa tonichini na vitamkwa kabla ya utekelezaji wa Sharti la Ukubalifu katika hatua ya mwisho ya ukokotozi kama inavyoelekezwa katika Nadharia ya FVH katika Makala haya. Hatuna budi kuendelea na uchanganuzi wa vitenzi vingine hususani vile vya silabi moja ya shina katika sehemu inayofuata:

Kwa ujumla ruwaza za toni katika vitenzi visoukomo sahili vya Kirombo zinaweza kuainishwa kwa kifupi kwenye jedwali kwa urahisi wa msomaji, kwa kuanza na Kiimbotoni Msingi, ruwaza za silabi mbili hadi silabi sita za shina la kitenzi kama ifuatavyo;

**Jedwali 2.** Muhtasari wa Ruwaza ya Toni katika Vitenzi Visoukomo Sahili vya Kirombo

| TJM | Silabi mbili | Silabi tatu | Silabi nne | Silabi tano | Silabi sita |
|---|---|---|---|---|---|
| CJC | CJC na CSC. | CJJC. | CJJJC, CJJCC na CCJJC | CJJJJC na CJJCJC | CJJJCJC |

Jedwali namba 2, linaonesha kwa kifupi muhtasari wa ruwaza za toni katika vitenzi visoukomo sahili vya Kirombo unavyojitokeza kwa kuanza na Tonijuu Msingi ambayo hupachikwa kwenye silabi ya kwanza ya shina kisha, ruwaza za ujitokezaji kwa kuanza na vitenzi vya silabi mbili hadi silabi sita za shina.

## 6. Hitimisho

Kwa hahika, tunaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa, ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika vitenzi visoukomo sahili vya silabi mbili hadi sita, toni J upachikwa kwenye silabi ya kwanza ya shina na kufuatiwa na ama toni J au toni C. Kanuni anuwai kama vile usambaaji wa TJM kuelekea kulia mwa shina la kitenzi, uhamaji wa TJM, uradidi wa TJM na Udondoshaji wa kitamkwa, zimetekelezwa baada ya utekelezwaji wa kanuni ya jumla ya Upachikaji wa TJM, katika uibuzi wa tabia ya ujitokezaji wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani. Aidha, ruwaza za ujitokezaji wa toni katika vitenzi vya idadi ya silabi mbili hadi sita vyote huanza na toni C katika KA ikifuatiwa ama na toni J au toni C katika silabi ya kwanza ya shina, toni J hiyo usambaa hadi silabi ya mwisho kasoro mbili au moja kutoka mwishoni mwa shina la vitenzi husika.

## Marejeleo


Batibo, H. M. (2012). Can tone shift be regarded as tone depression in Shisukuma? In M. Brenzinger & A.-M. Fehn (Eds.), *Proceedings of the 6th World Congress of African Linguistics* (pp. 201–206). Rüdiger Köppe Verlag.

Goldsmith, J. (1976). *Autosegmental phonology*. Unpublished doctoral dissertation, Massachusetts Institute of Technology.

Heine, B., & Nurse, D. (Eds.). (2000). *African languages: An introduction*. Cambridge University Press.

Hyman, L. M., & Byarushengo, E. R. (1984). A model of Haya tonology. In G. N. Clements & J. Goldsmith (Eds.), *Autosegmental studies in Bantu tone* (pp. 52–104). Foris Publications.

Ismail, J. H. (2011). *A tonological study of Meeto-Makua of Southern Tanzania* (Unpublished master's thesis). University of Dar es Salaam.

Ismail, J. H. (2016). *Uchambuzi wa toni kwa mbala wa kiinitoni na tonijuu msingi: Uchunguzi wa lugha ya Ki-Meetto-Makuwa cha Tanzania* (Mulika No. 35). University of Dar es Salaam.

Kothari, C. R. (2010). *Research methodology: Methods & techniques* (6th ed.). New Age International Publishers.

Marlo, M. R. (2007). The verbal tonology of Lunyala and Lumarachi: Two dialects of Luluyia (Bantu, J.30, Kenya). *Unpublished doctoral dissertation*, University of Michigan.

Martinet, A. (2005). *Économie des changements linguistiques*. Maisonneuve et Larousse.

Mashauri, M. A. (2012). Toni katika nomino za lugha ya Ki-Konongo. *Unpublished master's thesis*, University of Dar es Salaam.

Massamba, D. P. B. (1984). Tone in Ci-Ruuri. In G. N. Clements & J. Goldsmith (Eds.), *Autosegmental studies in Bantu tone* (pp. 235–254). Foris Publications.

Massamba, D. P. B. (2011). *Maendeleo katika nadharia ya fonolojia*. TATAKI.

McHugh, B. D. (2006). The phrasal cycle in Kivunjo Chaga tonology. In J. Inkelas & M. Zec (Eds.), *Theoretical issues in African linguistics* (pp. 217–242).

MLUTA. (2009). Retrieved April 10, 2018, from http://www.google.com/lugha/

Mramba, P. T. (2015). Athari za Kirombo katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili: Vipengee vya kifonolojia na kimofolojia. *Unpublished master's thesis*, University of Dar es Salaam.

Nelson, C. (2013). Toni katika vitenzi vya Kimochi. *Unpublished master's thesis*, University of Dar es Salaam.

Nurse, D., & Phillipson, G. (1977). Tones in Old Moshi (Chaga). *Studies in African Linguistics, 8*, 49–80.

Nurse, D., & Philippson, G. (Eds.). (2003). *The Bantu languages*. Routledge.

Odden, D. (1989). Predictable tone systems in Bantu. In H. van der Hulst & N. Smith (Eds.), *Autosegmental studies on pitch accent systems* (pp. 225–251). Foris.

Polomé, S. A. (1971). *Phonological survey of the Chaga dialect of Tanzania*. Unpublished master's thesis, University of Texas, Austin.

Raum, J. (1964). *Versuch einer Grammatik der Dschaggasprache (Moschi-Dialekt)*. The Gregg Press.

Van Spaandock, M. (1971). *L'analyse morphotonologique dans les langues bantoues*. SELAF.